

**NI YUPI RAFIKI MWEMA?**

الصديق الصالح

**IMEANDALIWA NA: YUNUS KANUNI  
NGENDA**

**IMEPITIWA NA: ABUBAKARI  
SHABANI RUKONKWA**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## Utangulizi

Ndugu zangu katika imani ni kawaida kwa binadam na ni muhim kuwa na rafiki, Lakini kwa Muislam kuchagua rafiki mzuri ni lazima kwa ajili ya kuhifadhi Dini yetu. Kufanya urafiki na watu wema wenyewe tabia nzuri, wenyewe dini na heshima ni moja ya mambo yanayotufanya sisi Waislam kuwa katika njia iliyonyooka, na kuwa mfano bora katika jamii.

Mtume (Swalla Allahu Alaihi Wa Sallam) amesema:

"Mtu yamkini (inawezekana) kufuata dini ya rafiki yake, kwa hivyo muangalie unayemfanya rafiki." {Abu Dawud na Tirmidhiy}

Ukiona rafiki yako ana matendo maovu, jaribu kumkumbusha,kumpa nasaha na mawaihda, asipobadilika na akaendelea kufanya maovu, ni vema kumuepuka kwa sababu unaweza ukaiga tabia zake ambazo zinakwenda kinyume na Dini yako (ya kiislam). Lakini pamoja na kumuepuka inakupasa kumfanyia wema na kumuombea kwa Allah uongofu.

Allah (Subhanahu Wa Ta'ala) amesema:

"Na Siku ambayo mwenye kudhulumu atajiuma mikono yake, na huku anasema: 'Laiti ningelishika njia pamoja na

Mtume (S.a.w) Ee Ole wangu! Laiti nisingelimpanya fulani kuwa rafiki! Amenipoteza nikaacha Ukumbusho, baada ya kwisha nijia, (kunijia) na kweli shetani ni khaini (mwenye khiyana)                                  kwa                                  mwanaadamu."  
{Surat Al-Furqaan 25:27-29}

Allah (Subhanahu Wa Ta'ala) tena Anasema:

"Siku hiyo marafiki watakuwa ni maadui, wao kwa wao, isipokuwa wachaji Allah (wacha Mungu)" {Surat Az-Zukhruf 43:67}

Muumini ni kioo cha ndugu yake muumini, akiona makosa ya mwenzake inampasa amueleze kwa uzuri na kumsaidia kurekebisha kosa hilo.

Huo ndio urafiki unaotakiwa katika Uislam, na muumini wa kweli lazima ataangalia nani wa kumfanya rafiki.

Lakini kwa masikitikiko makubwa vijana wa kiislam wa leo hawana habari na jambo kama hili, imefikia hatua marafiki wa zama hizi wanatumia muda mwingi kusaidiana katika mambo yasiyofaa, badala ya kusaidiana katika mambo ya dini na ya kheri.

Tunamuomba Allah atuongoze pamoja na marafiki zetu. Ameen!!!